

HALMASHAURI YA WILAYA YA SERENGETI

SHULE YA SEKONDARI NYANSURURA,

S. L. P 84,

MUGUMU-SERENGETI.

12/12/2020.

MZAZI/MLEZI.....

S.L.P.....

MUGUMU- SERENGETI.

Ndugu;

YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA-2021.

Napenda kukuarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule ya sekondari nyansurura 2021.

Nakutumia barua hii ili uweze kumuandaa mwanao vyema na masomo kwa faida yake na taifa kwa ujumla. Mwanao anatakiwa kufika shuleni mara tu shule ifunguliwapo mnamo tarehe 11/01/2021. Mzazi mpendwa unaombwa kufika shuleni mara upatapo barua hii kwa maelekezo Zaidi.

Asante.

Wako



SARAH G UISO.

MKUU WA SHULE

HEADMISTRESS
NYANSURURA SECONDARY

MAHITAJI YA SHULE

SARE YA SHULE.

Mwanao anatakiwa kuvaa sare ya shule wakati wote awapo shuleni isipokuwa pale atakapopewa ruhusa maalum na uongozi wa shule.

WAVULANA

1. Washone suruali mbili za rangi ya damu yam zee na nyeusi. Suruali iwe na marinda mawili kwa mbele na turn-up na isiwe ya kubana wala modo.
2. Mashati mawili [02] meupe ya mikono mifupi aina ya TOMATO.
3. Soksi jozi mbili rangi nyusi
4. Viatu vyeusi vyangozi vyenye visigino vifupi vya kufunga kwa kamba.
5. Sweta ya rangi ya kijani.
6. Nguo za michezo
 - T-Shirt rangi ya blue.
 - Bukta rangi ya blue
 - Raba za michezo[muhimu kwa maendeleo ya afya yake]
 - Track- suit rangi njano yenye michilizi miyeupe miwili pembeni.

WASICHANA

1. Washone sketi mbili [02] za rangi ya damu ya mzee na nyeusi zenye marinda ya kulaliana 16 zenye urefu unaovuka goti[hakikisha sketi ya mwanao ni ndefu kuepuka usumbufu wa kurudia kushona sketi].
2. Mashati mawili[02] meupe ya mikono mifupi aina ya TOMATO[Sketi au mashati ya mtumba hayatakubalika]
3. Viatu vyeusi vya ngozi vyenye visigino vifupi vya kufunga kwa kamba.
4. Soksi jozi mbili ndefu nyeupe.
5. Nguo za michezo:
 - T-shirt rangi ya blue
 - Raba za michezo[muhimu kwa maendeleo ya afya yake]
 - Track suit rangi ya njano yenye michilizi miyeupe miwili pembeni[nzito na isiyobana]

VIFAA VINGINE MUHIMU

1. Madaftari makubwa [counter book 9] na Ream [01] double A.
2. Mathematical set[BOFA] Lenye vifaa ndani yake.

3. Kamusi na dictionary ni muhimu kwa maendeleo yake ya kitaaluma.

4. KITI NA MEZA KWA MWANAO NI LAZIMA.

5 .JEMBE 01 na mpini wake kwa wavulana.

6. NDOO LITRE 20 kwa wasichana.

KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sharia ya elimu na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sharia na. 10 ya mwaka1995. Aidha,inazingatia miongozo yote inayotolewa na ofisi Raisi-Tawala za mikoa na serikali za mitaa, yenye dhamana na jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu.Unatakiwa kuzingatia mambo muhimu yafuatayo:

1. Heshima kwa viongozi,wazazi,wafanyakazi wote,wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla.
2. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani nan je ya shule kulingana na ratiba ya shule.
3. Kuwahi shuleni na katika shughuli za shule na shughuli zingine utakazopewa.
4. Kufahamu mipaka ya shule vizuri.
5. kutunza usafi mwili,mavazi na mazingira ya shule.
6. Kutunza mali ya umma na kujiepusha katika wizi na mali ya umma kama vile vitabu,viti, na meza za shule.
7. Kuwa na bidii katika masomo ambayo ndicho kiini cha uanafunzi waako.
8. kushirikiana vyema na wenzako katika kufanikisha lengo kuu la shule na serikali.

MAKOSA YAFUATAYO YANAWENZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE:

- A. WIZI
- B. Uasherati ushoga
- C. Ubakaji
- D. ulevi matumizi ya dawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, mirungi,kuberi na kadhalika.
- E. kupiga au kupigana
- F. kuharibu kwa makusudi na mali ya umma.
- G. kudharau bendera ya taifa au wimbo taifa
- H. kuwa mjamzito/ kupata mimba,kusababisha mimba na kutoa.
- I. kugoma/kugomea adhabu kwa makusudi.
- J. kugoma ,kuchoche na kuongoza au kushiriki kuvuruga Amani na usalama wa shule na watu.
- K. kumiliki au kukutwa na simu ya mkononi.
- L. utoro wa kuanzia siku 90 utakuondoa shuleni.
- M. kuoa au kuolewa ni marufuku.

MOTO WA SHULE

RISE AND SHINE

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

.....
SARAH G UISO

MKUU WA SHULE

HEADMISTRESS
NYANSURURU SECONDARY

PRESIDENT'S OFFICE REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL
GOVERNMENT

MEDICAL EXAMINATION FORM

Full name.....

Age.....Height.....weight.....

1. Blood count.....(red and White).....
2. Stool Examination,.....
3. Urinalysis.....
4. Syphilis and other V.D.....
5. T.B and Leprosy Test.....
6. Eyes Test.....
7. Ears Test.....
8. Chest Test.....
9. Abdomen Test.....
10. Plano Test (for girls).....
11. Spleen.....

Additional information e.g. physical defects or impairments ,infections, chronic or family disease (e.g. circle cell anemia), inability to eat certain foods etc.

.....
.....
.....

I certify that the above named student is fit/ is Not fit to pursue secondary education.

Signature.....

Designation.....

Station.....

Date.....